HOTUBA YA WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO MHESHIMIWA PROF. MAKAME M. MBARAWA (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

A. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika***, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

2. ***Mheshimiwa Spika***, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na kutuwezesha sote kukutana tena leo kujadili maendeleo ya Sekta za Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

3. ***Mheshimiwa Spika***, napenda nimpongeze kwa namna ya pekee Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa umahiri mkubwa na kudumisha umoja, amani na utulivu. Mheshimiwa Rais ameendelea kusimamia utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu ya mwaka 2015 na kutekeleza kwa kiwango kikubwa ahadi za Serikali kwa wananchi. Ama kwa hakika uongozi wake mahiri umekuwa

dira sahihi katika kuleta ***mabadiliko ya kweli*** ambayo Watanzania wameyasubiri kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, pia, nawapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu kwa jinsi ambavyo wamemsaidia Mheshimiwa Rais kusimamia na kuongoza shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nikupongeze wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuliongoza Bunge hili Tukufu kwa hekima na busara.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka huu mmoja tangu Bunge la Bajeti lililopita, Bunge lako Tukufu limepata pigo kubwa kwa kuondokewa na wapendwa wetu Mhe. Hafidh Ally Tahir, Mbunge wa Dimani na Mhe. Dkt. Elly Marko Macha, Mbunge wa Viti Maalum. Naomba kutoa salamu zangu za pole na kumwomba Mwenyezi Mungu aendelee kutupa sote moyo wa subira.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda pia kuwapongeza Mhe. Prof. Palamagamba Kabudi, Mhe. Anne Killango Malecela, Mhe. Alhaj Abdallah Majura Bulembo, Mhe. Salma Rashid Kikwete na Mhe. Mchungaji Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare kwa kuteuliwa kuwa Wabunge wa Bunge hili. Aidha, nimpongeze Mhe. Juma Ali Juma kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Mbunge wa Jimbo la Dimani.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** sina budi kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Prof. Norman Adamson Sigalla King, Mbunge wa Jimbo la Makete na Makamu

Mwenyekiti Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Vijijini kwa kuendelea kunipa ushirikiano wa kutosha katika kuiongoza Wizara yangu.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) kwa hotuba yake iliyotoa Tarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa mwaka 2016/17 na Mwelekeo wa Kazi za Mwaka wa fedha 2017/18. Nawapongeza pia Waheshimiwa Mawaziri wote walionitangulia kuwasilisha hoja zao katika Bunge lako la Bajeti.

B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE KWA MWAKA 2016/2017

C.1.1 SEKTA YA UJENZI

8. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Sekta ya Ujenzi ilitengewa kiasi cha **Shilingi bilioni 35.941** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2017 **Shilingi bilioni 25,786** zilikuwa zimetolewa na HAZINA.

9. ***Mheshimiwa Spika***, Aidha, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Sekta ya Ujenzi ilitengewa **Shilingi Trilioni 2.176** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali ni **Shilingi Trilioni 1.248** na **Shilingi bilioni 344.838** zilikuwa fedha za nje. Kwa upande wa fedha za Mfuko wa Barabara zilitengwa ni **Shilingi bilioni 582.644**. Hadi Aprili, 2017 fedha zilizotolewa ni **Shilingi Trilioni 1.171**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi**

bilioni 958.528 ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 212.793** ni fedha za nje. Fedha za ndani zilizotolewa zinajumuisha **Shilingi bilioni 455.215** za Mfuko wa Barabara. Kwa ujumla, kiasi kilichotolewa ni sawa na asilimia 53.8 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

i. Barabara na Madaraja

10. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutekeleza sera ya kuunganisha mikoa yote na nchi zote jirani kwa barabara za lami. Miradi ya barabara yenye jumla ya takriban kilometa 987 na madaraja makubwa mawili ilikamilika kujengwa na kukarabatiwa kwa kiwango cha lami katika mwaka wa fedha 2016/2017. Miradi hiyo iliyokamilika ni pamoja na ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara ya Namtumbo – Kilimansera – Matemanga - Tunduru (km 187.9); Tunduru – Nakapanya – Mangaka (km 137.3) na Mangaka – Mtambaswala (km 65.5) katika Ukanda wa Kusini. Kwa upande wa Ukanda wa Kaskazini, miradi iliyokamika ni ukarabati wa barabara ya Mkumbara – Same (km 96) na ujenzi wa barabara ya Dodoma – Babati (sehemu ya Dodoma – Mayamaya - km 43.65). Kwa upande wa Ukanda wa Kati, Magharibi na Ukanda wa Ziwa miradi iliyokamilika ni ujenzi wa barabara ya Mbeya – Lwanjilo – Chunya (km 72), barabara ya Mwigumbi – Maswa – Bariadi – Lamadi (sehemu ya Bariadi – Lamadi - km 71.8), barabara ya Nzega – Puge (km 58.8), barabara ya Sitalike – Mpanda (km 36.9), barabara ya Tabora – Urambo - Ndono (km 94) na barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo (sehemu ya Kyaka - Bugene (km 59.1). Kwa upande wa Ukanda wa Mashariki, ujenzi wa barabara ya Bagamoyo – Msata (km 64) umekamilika kwa kiwango cha lami. Madaraja makubwa yaliyokamilika ni Daraja la Kilombero na Daraja la Ruvu Chini.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu utekelezaji wa kazi zilizopangwa kwa mwaka 2016/17, hadi kufikia Machi, 2017, **kilometa 433** za barabara kuu zilikamilika kujengwa kwa kiwango cha lami kati ya lengo la **kilometa 592.** Aidha, ukarabati wa jumla ya **kilometa 77** kati ya lengo la **kilometa 146.5** za barabara kuu kwa kiwango cha lami ulikamilika.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa matengenezo ya barabara, matengenezo ya barabara kuu na barabara za mikoa yalihusisha matengenezo ya kawaida *(routine and recurrent maintenance)* **kilometa 22,839**, matengenezo ya muda maalum na sehemu korofi **kilometa 4,749** na matengenezo ya madaraja **2,821**. Hadi kufikia Machi, 2017, kwa ujumla, utekelezaji wa mpango wa matengenezo ya barabara ulikuwa umefikia **asilimia 67** ya malengo ya mwaka wa fedha 2016/2017 ambapo katika barabara kuu, jumla ya **kilometa 5,895.31** zilifanyiwa matengenezo ya kawaida, **kilometa 1,074.5** zilifanyiwa matengenezo ya muda maalum na sehemu korofi na madaraja **998** yalifanyiwa matengenezo. Kwa upande wa barabara za mikoa, jumla ya **kilometa 12,746.90** zilifanyiwa matengenezo ya kawaida, **kilometa 1,745.2** zilifanyiwa matengenezo ya muda maalum na sehemu korofi na madaraja **1,032** yalifanyiwa matengenezo.

13. ***Mheshimiwa Spika***, maelezo zaidi kuhusu utekelezaji wa miradi ya barabara na madaraja katika mwaka wa fedha 2016/2017 yamo katika **ukurasa wa 9 hadi 49** wa Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

ii. Taasisi Zilizo Chini ya Sekta ya Ujenzi

14. ***Mheshimiwa Spika,*** maelezo kuhusu utendaji wa Taasisi zilizo chini ya Sekta ya Ujenzi yameoneshwa kwa kina katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti kuanzia **ukurasa wa 49 hadi 67**.

C.1.2 SEKTA YA UCHUKUZI

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/2017, Sekta ya Uchukuzi iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi Trilioni 2.587** kati ya hizo, **Shilingi trilioni 2.495** ni fedha za Maendeleo na **Shilingi bilioni 91.519** ni fedha za Matumizi ya Kawaida. Hadi Aprili, 2017, fedha za Miradi ya Maendeleo **Shilingi bilioni 825.858,** sawa na asilimia 33.1 zilikuwa zimetolewa na fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi bilioni 58.739** sawa na asilimia 64.18 zilikuwa zimetolewa.

Usafiri kwa Njia ya Barabara

15. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia SUMATRA imeendelea kusimamia na kudhibiti utoaji wa huduma za uchukuzi Majini na vijijini kwa kufanya kaguzi za kushtukiza za vyombo vya usafiri; utoaji nauli elekezi, elimu na mafunzo; na ushauri kwa watumiaji na watoaji wa huduma za usafiri wa barabara.

Usafiri wa Reli Jijini Dar es Salaam

16. ***Mheshimiwa Spika,*** huduma za usafiri wa reli katika Jiji la Dar es Salaam zimeendelea kutolewa na TAZARA na TRL. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, idadi ya watumiaji wa usafiri wa treni Jijini Dar es Salaam ilikuwa abiria 5,762,555 ikilinganishwa na abiria 1,771,188 waliosafiri katika kipindi kama hicho mwaka 2015/2016. Hili

ni ongezeko la asilimia 225. Maelezo zaidi kuhusu usafiri wa reli Jijini Dar es Salaam yapo kwenye **Kitabu changu cha Hotuba kuanzia ukurasa wa 73 hadi 74**.

Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli (RAHCO), Kampuni ya Reli Tanzania (TRL) na TAZARA

17. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, kazi za kuboresha, kujenga, kukarabati miundombinu ya reli na upembuzi yakinifu zimeendelea kutekelezwa na RAHCO, TRL na TAZARA kwa niaba ya Serikali. Kazi zilizofanyika ni pamoja na:

i. Kusaini mkataba wa ujenzi wa reli ya Kati kwa kiwango cha *standard gauge* kutoka Dar es salaam hadi Morogoro. Mkataba huo ulisainiwa tarehe 3 Februari 2017. Aidha, tarehe 12 Aprili, 2017, Rais ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa John Pombe Magufuli aliweka jiwe la msingi kwa ajili ya kuanza ujenzi wa reli hiyo;

ii. Zabuni ya ujenzi wa reli ya Kati kwa kiwango cha *standard gauge* kutoka Morogoro mpaka Makutupora (Km 336) zimefunguliwa na evalution inafanyika.

iii. Zabuni kwa ajili ya kuwapata Wakandarasi wa ujenzi wa reli ya Kati kwa kiwango cha *standard gauge* kutoka Makutupora hadi Tabora; Tabora hadi Isaka; na Isaka hadi Mwanza zitafunguliwa mwisho wa mwezi huu.

iv. Kwa Upande wa TAZARA: Matengenezo makubwa ya njia ya reli yamefanyika ili kupunguza maeneo korofi.

Maelezo zaidi kuhusu kazi zilizotekelezwa na RAHCO, TRL na TAZARA yapo katika **Kitabu changu cha Hotuba kuanzia ukurasa wa 74 hadi 79**.

USAFIRI NA UCHUKUZI MAJINI

Huduma za Uchukuzi Katika Maziwa

18. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Serikali ilitenga fedha Shilingi bilioni 50.5 kwa ajili ya kununua meli moja (1) katika ziwa Victoria na kukarabati meli tatu (3). Kuhusu ujenzi wa meli mpya katika Ziwa Victoria, taratibu za kumpata Mkandarasi zinatarajiwa kukamilika Mei 2017 na kuhusu Mradi wa ukarabati wa MV.Liemba, mkandarasi amepatikana na kazi hii inatarajiwa kuanza Mei, 2017. Maelezo zaidi kuhusu kazi zilizotekelezwa na MSCL yapo katika **Kitabu changu cha Hotuba kuanzia ukurasa wa 81 hadi 83**.

Huduma za Bandari

19. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/17 TPA ilichukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufungua ofisi za huduma za bandari katika miji ya Lubumbashi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DR Congo), Lusaka (Zambia), Kigali (Rwanda) na Bujumbura (Burundi); kuanzisha wakala wa Mamlaka huko Kampala, Uganda; kuimarisha usalama wa mizigo bandarini na kutoa huduma za bandari kwa saa 24 kwa siku na siku 7 kwa wiki.

20. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi ya kuboresha utendaji wa bandari za Mwambao na Maziwa Makuu iliyotekelezwa katika mwaka 2016/2017 ni pamoja na:

i. Kukamilika kwa jengo la ghorofa 35 la kuwaweka pamoja wadau muhimu wanaotoa huduma katika Bandari ya Dar es Salaam (One Stop Center). Jengo hilo lilizinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Mheshimiwa Joseph Kabila tarehe 4 Oktoba, 2016;

ii. Kukamilisha Upembuzi Yakinifu wa uboreshaji wa bandari ya Dar es Salaam Machi, 2017. Kazi za ujenzi zinatarajiwa kuanza Juni, 2017;

iii. Ujenzi wa gati la Kagunga katika Ziwa Tanganyika ulikamilika Januari, 2017;

iv. Ujenzi wa gati la Ntama katika Ziwa Victoria ulikamilika Agosti, 2016;

v. Ujenzi wa gati la Lushamba ulikamilika Julai 2016;

vi. Ujenzi wa Meli yenye uwezo wa kubeba abiria 200 na tani 200 za mizigo katika Ziwa Nyasa ulianza Juni, 2016 na unatarajiwa kukamilika Agosti 2017;

vii. Ukarabati wa gati la Lindi umekamilika kwa asilimia 50. Kazi inatarajiwa kukamilika Agosti, 2017;

viii. Ujenzi wa gati la Pangani ulikamilika Septemba, 2016.

ix. Kazi ya kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ya Karema, Kigoma ili kuunganishwa na Bandari ya Kalemie, DRC inaendelea. Kazi za ujenzi zinatarajiwa kuanza Septemba 2017.

21. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea na maandalizi ya msingi ya ujenzi wa bandari ya Mbegani, Bagamoyo. Kwa sasa majadiliano na Kampuni ya China Merchants Port Limited (CMPort) kuhusu vipengele vya Mikataba yanakamilishwa.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu ujenzi wa bandari ya Mwambani, Tanga, TPA inaendele maandalizi ya makabrasha kwa ajili ya marejeo ya upembuzi yakinifu na zabuni hiyo inatarajiwa kutangazwa kabla ya Juni 2017. Aidha, maandalizi kwa ajili ya kujenga gati la Chongoleani (Tanga) kwa ajili ya kupokelea mafuta kutoka Uganda yanaendelea kwa kufanya upembuzi yakinifu.

23. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu upanuzi wa Bandari ya Mtwara, awamu ya kwanza inahusu ujenzi wa gati moja ambapo Kampuni ya *China Railway Construction Company (CRCC)* ilisaini Mkataba wa ujenzi tarehe 4 Machi, 2017. Gati hilo lenye urefu wa mita 350 ni kwa ajili ya kuhudumia shehena mchanganyiko. Ujenzi wa gati hili utakamilika ndani ya miezi 21.

Maelezo zaidi kuhusu miradi na huduma za bandari yapo katika **Kitabu changu cha Hotuba kuanzia ukurasa wa 83 hadi 94**.

USAFIRI NA UCHUKUZI KWA NJIA YA ANGA

Udhibiti wa Usalama wa Usafiri wa Anga

24. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA) iko katika hatua ya mwisho kumpata Mkadarasi kwa ajili ya

ununuzi wa Rada 4 kwa ajili ya Viwanja vya ndege vya JNIA, Mwanza, KIA na Songwe. Aidha, hadi Aprili, 2017, Tanzania imeingia mikataba ya BASA na jumla ya nchi 68 ikilinganishwa na nchi 60 zilizokuwa zimesaini makubaliano hayo mwaka 2015/2016. Maelezo zaidi kuhusu udhibiti wa Usafiri wa Anga yapo katika **Kitabu changu cha Hotuba kuanzia ukurasa wa 94 hadi 99**.

Huduma za Viwanja vya Ndege

25. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) imeendelea kuboresha miundombinu na huduma za viwanja vya ndege nchini ili kuwezesha ndege kubwa na ndogo kutua na kuruka kwa usalama. Miradi iliyotekelezwa ni pamoja na:-

i. Ujenzi wa jengo la tatu la abiria (Terminal III) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA) unaendelea kutekelezwa na unatarajiwa kukamilika Desemba 2017. Kukamilika kwa jengo hilo kutaongeza uwezo wa kiwanja kuhudumia hadi abiria milioni 8.5 kwa mwaka kutoka abiria milioni 2.5;

ii. Ukarabati wa kiwanja cha KIA umekamilika kwa asilimia 70 na ujenzi unatarajiwa kukamilika Mei, 2017.

iii. Kukamilika kwa kazi za kurefusha barabara ya kuruka na kutua ndege kwa mita 500 katika kiwanja cha Mwanza. Kazi zinazoendelea ni ujenzi wa jengo la kuongozea ndege, ujenzi wa jengo la mizigo na maegesho ya ndege;

iv. Awamu ya pili ya ukarabati na uboreshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Tabora inaendelea. Kazi za ukarabati wa Kiwanja hiki zilianza Septemba, 2016 na zinatarajiwa kukamilika Juni, 2017; na

v. Kukamilika kwa ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Bukoba na kuanza kutumika. Aidha, ujenzi wa shule ya Msingi kwa ajili ya kupisha mradi huu umekamilika Aprili, 2017.

Maelezo zaidi kuhusu huduma za viwanja vya ndege yapo katika **Kitabu changu cha Hotuba kuanzia ukurasa wa 100 hadi 103**.

Huduma za Usafiri wa Anga

26. ***Mheshimiwa Spika,*** huduma za usafiri wa anga ndani na nje ya nchi zimeendelea kutolewa na Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) pamoja na Kampuni za sekta binafsi.

27. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutekeleza azma yake ya kufufua na kuboresha huduma za Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL) ili kusaidia kukuza sekta nyingine za kiuchumi ikiwa ni pamoja na utalii, biashara, madini na kilimo. Katika mwaka 2016/2017, Serikali iliingia mikataba ya ununuzi wa ndege sita. Ndege mbili (2) aina ya *Bombardier Dash 8 – Q400* zenye uwezo wa kubeba abiria 76 kila moja ziliwasili nchini Septemba, 2016 na kuanza kazi Oktoba 2016. Ndege moja (1) aina ya *Bombardier Dash 8 – Q400* itawasili nchini Julai, 2017; ndege mbili (2) aina ya *Bombardier CS 300* zenye uwezo wa kubeba abiria 127 kila moja zitawasili nchini Juni, 2018 na ndege moja (1) ya masafa marefu aina ya *Boeing 787 Dreamliner* yenye uwezo wa kubeba abiria 262 itawasili nchini Julai, 2018. Maelezo zaidi kuhusu huduma za Usafiri wa Anga yapo katika **Kitabu changu cha Hotuba kuanzia ukurasa wa 104 hadi 106**.

C.1.3 SEKTA YA MAWASILIANO

28. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2016 hadi mwezi Aprili, 2017, Wizara iliweza kukusanya kiasi cha Dola za Marekani **milioni 6.577** (sawa na **Shilingi bilioni 14.260**) kutokana na Mradi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, ambapo fedha hizo ni maalum kwa ajili ya urejeshaji/ulipaji wa deni la ujenzi wa mradi huo kwa Benki ya EXIM ya China na pia kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa Mkongo huo.

29. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Sekta ya Mawasiliano ilitengewa kiasi cha **Shilingi bilioni 3.073** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2017 **Shilingi bilioni 2.262** zilikuwa zimetolewa na HAZINA.

30. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2016/2017, Sekta ya Mawasiliano ilitengewa jumla ya **Shilingi bilioni 92.730** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani ni **Shilingi bilioni 5.00** na **Shilingi bilioni 87.73** zilikuwa fedha za nje. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2017 fedha zilizopokelewa ni **Shilingi bilioni 37.295.**

i. Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mawasiliano inaratibu na kusimamia utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

nchini, ambao kwa mwaka wa fedha 2016/17 ilifikia Awamu ya III sehemu ya kwanza na IV ya utekelezaji. Awamu ya III sehemu ya kwanza ilihusisha uunganishaji wa Zanzibar katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, ujenzi wa mtandao wa miundombinu ya Itifaki [Internet Protocol-Multilayer Label Switching) na ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Data (National Internet Data Centre). Awamu hiyo ilikamilika mwezi Julai, 2016 na kuanza kufanya kazi ya kutoa huduma. Hadi sasa kuna wateja 27 ambao wameanza kutumia kituo hicho.

Awamu ya IV ni ujenzi wa mikongo ya mijini (Metro Networks) unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali na Watoa Huduma za Mawasiliano (Tigo, Airtel na Zantel).

ii. Juhudi za Serikali Kufikisha Huduma ya Mawasiliano Vijijini

31. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Mawasiliano kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) kwa kushirikiana na watoa huduma za mawasiliano katika mwaka wa fedha 2016/2017, imeendelea na ufikishaji wa huduma ya mawasiliano vijijini ambapo mpaka sasa jumla ya kata 382 kati ya kata 443 zenye vijiji 1,825 na wakazi 2,891,731 zimekwisha pata huduma ya mawasiliano. Serikali inawahimiza watoa huduma wote ambao hawajakamilisha miradi ya kufikisha huduma za mawasiliano vijijini kufanya hivyo mara moja bila ucheleweshaji zaidi.

iii. Programu ya Miundombinu ya TEHAMA ya Kikanda (RCIP)

32. ***Mheshimiwa Spika***, Sekta ya Mawasiliano inatekeleza Programu ya Miundombinu ya TEHAMA ya Kikanda (RCIP) kwa kutumia fedha za nje. Miradi inayotekelezwa ni pamoja na:- Mradi wa shule mtandao (e-school) unaohusisha ununuzi, usimikaji na ufungaji wa vifaa vya TEHAMA katika Shule 80 za Sekondari na kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa walimu walioteuliwa kwa kazi hiyo katika shule hizo. Pia Mradi wa *Video Conference:* unaohusisha ununuzi, ufungaji na usimikaji wa mitambo ya video conference katika Makao Makuu ya Mikoa 26 na baadhi ya Taasisi za Serikali unaendelea.

33. ***Mheshimiwa Spika,*** Programu nyengine za RCIP inatelekelezwa kwa kushirikisha taasisi nyingine za Serikali.

34. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa Majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Sekta ya Mawasiliano (UCSAF, TCRA, TPC, TTCL na Tume ya TEHAMA) umeoneshwa kwenye **ukurasa 117 hadi 125** wa Kitabu changu cha Hotuba ya Bajeti.

C. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

F.1 SEKTA YA UJENZI

35. ***Mheshimiwa Spika,*** bajeti ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara (Fungu 98 - Ujenzi) kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ni **Shilingi bilioni 34.123** Aidha, Sekta ya Ujenzi imetengewa jumla ya **Shilingi trilioni 1.895** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi trilioni 1.350** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 545.582** ni

fedha za nje. Aidha, kati ya fedha za ndani **Shilingi bilioni 642.284** ni fedha zilizotengwa kwa ajili ya bajeti ya Mfuko wa Barabara. Mgawanyo huo umeonesha kwenye ***Kiambatisho Na.1*** **ukurasa wa 214 hadi 250** katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti. Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo ni kama ifuatavyo:

Miradi ya Barabara na Madaraja

36. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2017/2018 jumla ya **Shilingi trilioni 1.052** kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara kuu zenye urefu wa **kilometa 720** kwa kiwango cha lami, ujenzi wa madaraja **13** pamoja na ukarabati wa **kilometa 150** kwa kiwango cha lami. Aidha, **Shilingi bilioni 30** kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali zimetengwa kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara za mikoa zenye urefu wa **kilometa 58.4** na madaraja **12** pamoja na ukarabati kwa kiwango cha changarawe wa **kilometa 469.5.**

37. ***Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya miradi ya barabara kuu inayoendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami itakayotekelezwa katika mwaka 2017/18 itahusisha barabara za Mayamaya – Mela – Bonga (km 188.2), Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 112), Sumbawanga – Kanazi (km 75), Kanazi – Kizi – Kibaoni (km 76.6), Kidahwe – Kasulu (km 50), Kibondo – Nyakanazi (km 50), Mafinga – Igawa (137.9), Arusha – Tengeru pamoja na barabara ya mchepuo ya Arusha (km 56.5), Makutano – Natta – Mugumu (km 50), Mwigumbi – Maswa (km 50), Bulamba –Kisorya (km 51), Sanya Juu – Alerai (km 32), Mtwara – Mnivata (km 50) na Mpanda – Ifukutwa – Vikonge (km 35). Aidha, ujenzi

kwa kiwango cha zege wa barabara ya Itoni – Ludewa – Manda sehemu ya Lusitu – Mawengi (km 50) utaendelea. Serikali itaanza pia utekelezaji wa miradi mingine ya barabara na madaraja ambayo inajumuisha barabara ya Tabora – Koga – Mpanda (km 343), Mbinga – Mbamba Bay (km 66), Masasi – Nachingwea – Nanganga (km 91), Chaya – Nyahua (km 85.4), Uvinza – Malagarasi (km 51.1), Njombe – Ndulamo - Makete (km 109), Mto wa Mbu – Loliondo sehemu ya Waso - Sale (km 49), Natta – Mugumu (km 41.6), Urambo – Kaliua (km 28), Kidatu – Ifakara (km 68), Kibaoni – Sitalike (km 71), Nyamuswa – Bunda – Bulamba (km 55), Mpemba – Isongole (km 51.2), Rujewa – Madibira – Mafinga (km 152), Njombe – Lupembe – Madeke (km125), Chunya – Makongolosi (km 43), Makongolosi – Rungwa – Itigi – Mkiwa (Sehemu ya Noranga – Itigi – Mkiwa, km 56.9) na Maswa – Bariadi (km 49.7). Aidha, katika mwaka 2017/18, Serikali itaanza ujenzi wa madaraja mapya ya Wami (Pwani), Selander (DSM), Magara (Manyara), Ukarabati wa Daraja la Kirumi (Mara) pamoja na kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Daraja la Simiyu, Kigongo - Busisi (Mwanza) na Daraja la Mtera (Dodoma).

38. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara itaendelea na ujenzi wa barabara za juu kwenye makutano ya TAZARA pamoja na ujenzi wa barabara ya Dar es Salaam – Chalinze kwa kiwango cha *Expressway*. Aidha, kufuatia kukamilika kwa Awamu ya Kwanza ya ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT), Serikali itaanza ujenzi wa Awamu zinazofuata za miundombinu ya BRT. Katika Awamu ya Pili, ujenzi utahusisha barabara za Kilwa, Kawawa na Chang'ombe zenye urefu wa kilometa 20.3 na ujenzi wa *flyovers* katika makutano ya Chang'ombe na Uhasibu chini ya ufadhili

wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Vilevile, Serikali itaanza utekelezaji wa mradi wa uboreshaji wa usafiri katika Jiji la Dar es Salaam *(Dar es Salaam Urban Transport Improvement Project)*. Mradi huo utahusisha ujenzi wa barabara za juu (*Interchange*) kwenye makutano ya Ubungo, ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) Awamu ya Tatu na Awamu ya Nne. Awamu ya Tatu itahusisha barabara za Azikiwe, Bibi Titi, Uhuru na Nyerere zenye urefu wa kilometa 23.6 kutoka katikati ya Jiji la Dar es Salaam hadi Gongo la Mboto. Awamu ya Nne itahusisha barabara za Ali Hassan Mwinyi, Sam Nujoma na Bagamoyo kutoka katikati ya Jiji la Dar es Salaam hadi Tegeta.

Maelezo ya kina kuhusu miradi ya barabara na madaraja itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2017/2018 yameoneshwa katika **ukurasa wa 146 hadi 166** katika Kitabu changu cha Hotuba ya Bajeti. Aidha, orodha ya miradi ya barabara za mikoa itakayotekelezwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 2 ukurasa wa 251 hadi 271.**

Ujenzi wa Miundombinu ya Viwanja vya Ndege

39. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara imepanga kujenga na kukarabati miundombinu ya viwanja vya ndege nchini ambapo jumla ya **Shilingi milioni 176,368.640** zimetengwa. Katika mwaka wa fedha 2017/18 Serikali itaendelea na ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria (TB III) katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Mwanza, ukarabati wa Uwanja wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) na ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Mkoa wa Geita. Aidha, Serikali itaanza upanuzi wa ujenzi wa viwanja vya ndege vya Tabora, Kigoma, Sumbawanga na Shinyanga.

Vilevile Serikali itaanza ukarabati na ujenzi wa viwanja vya ndege vya Mtwara, Musoma, Iringa na Songea. Maelezo ya kina kuhusu kazi zitakazofanyika yapo katika ukurasa wa **168 hadi 174** wa Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

Fedha za Mfuko wa Barabara

40. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2017/2018, Mfuko wa Barabara unatarajiwa kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 917.548** zitakazotumika kufanya kazi za matengenezo ya barabara nchini. Kati ya fedha hizo, Sekta ya Ujenzi na Taasisi zake imetengewa **Shilingi bilioni 642.284** na Ofisi ya Rais – TAMISEMI imetengewa **Shilingi bilioni 275.264**.

41. ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya **Shilingi bilioni 642.284** zilizotengwa kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi) imetengewa **Shilingi bilioni 63.676** kwa ajili ya kazi za ukarabati wa barabara, kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara, ukarabati na ununuzi wa vivuko. Mchanganuo wa miradi hiyo umeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 3 ukurasa wa 272 hadi 282** wa Kitabu cha Hotuba ya Bajeti. Aidha miradi ya barabara za mikoa itakayotekelezwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 4 ukurasa wa 283 hadi 298** wa Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

42. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala wa Barabara umetengewa Shilingi **bilioni 573.084** kwa ajili ya matengenezo ya barabara kuu na barabara za mikoa. Muhtasari na maelezo ya kina ya mpango wa matengenezo ya

barabara na madaraja kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara yapo katika **Viambatisho Na. 5, 5A – 5E ukurasa wa 299 hadi 380** katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

43. ***Mheshimiwa Spika,*** maelezo ya kina kuhusu mpango wa utekelezaji kazi katika Taasisi zilizo chini ya Sekta ya Ujenzi katika mwaka wa fedha 2017/2018 yametolewa katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara **ukurasa 177 hadi 185.**

F.2 SEKTA YA UCHUKUZI

Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2017/18

44. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka wa fedha 2017/2018, bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Sekta ya Uchukuzi ni **Shilingi bilioni 91.142.** Aidha, Sekta ya Uchukuzi imetengewa jumla ya **Shilingi trilioni 2.477** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Mgawanyo wa fedha za maendeleo pamoja na miradi iliyotengewa fedha ni kama inavyooneshwa katika ***Kiambatisho Na.6.*** Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo ni kama ifuatavyo:

45. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Sekta ya Uchukuzi imepanga kutekeleza miradi ifuatayo:

i. Kuendelea na ujenzi wa reli ya Kati kwa sehemu ya Dar es Salaam hadi Dodoma kwa kiwango cha *standard gauge* ambapo Shilingi bilioni 900 zimetengwa;

ii. Kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa njia ya reli kati ya Mtwara – Mbamba Bay na matawi ya Mchuchuma na Liganga. Shilingi bilioni 2.00 zimetengwa;

iii. Shilingi bilioni 1.00 zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa reli kati ya Arusha – Musoma;

iv. Kukarabati njia ya reli kutoka Dar es Salaam hadi Isaka. Kazi hizi zinagharamiwa na Benki ya Dunia ambapo Shilingi bilioni 200 zimetengwa; n.k.

46. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuboresha huduma za uchukuzi wa abiria na mizigo katika Maziwa Makuu, katika mwaka 2017/2018, Serikali imetenga **Shillingi bilioni 24.496** kwa ajili ya Ujenzi wa Meli mpya na ubarabati wa meli ziliopo.

47. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu miradi ya miundombinu ya bandari, Serikali kupitia TPA imetenga **Shilling bilion 487.281** kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali.

48. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2017/2018, Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL) imetengewa shilingi bilioni 500 kwa ajili ya kukamilisha malipo ya ununuzi wa ndege 3 ambapo ndege mbili (2) ni za aina ya CS 300 na ndege kubwa moja (1) ya masafa marefu aina ya Boeing 787-8 Dreamliner. Fedha hizo pia zitatumika kwa ajili ya gharama za bima, mafunzo (marubani, wahandisi na wahudumu), gharama za kuanzia (start up cost) pamoja na malipo ya awali ya ndege nyingine ya aina ya Boeing 787 (Dreamliner). Aidha,

katika mwaka 2017/2018, Serikali imetenga Shilingi bilioni 10.00 kwa ajili ya kufanyia matengenezo ndege 4 za Serikali.

49. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Sekta ya Uchukuzi kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imetengewa Shilingi bilioni 5, kwa ajili ya ununuzi na usimikaji wa vifaa vya usalama viwanjani. Aidha, Mamlaka ya Hali ya Hewa imetengewa Shilingi bilioni 6.2 kwa ajili ya ununuzi wa Rada na vifaa vya hali ya hewa na TCAA itagharamia ununuzi na ufungaji wa Rada nne (4) za kuongozea ndege za kiraia.

50. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendelea kuboresha miundombinu ya Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA), jumla ya Shilingi bilioni 26.00 zimetengwa. Aidha, Serikali itaendelea kuboresha huduma zinazotolewa na Kampuni ya Reli (TRL) ambapo Shilingi bilioni 30.80 zimetengwa. Kazi zitakazotekelezwa na TRL na TAZARA zimeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti, ukurasa wa 195 na 196.

Mgawanyo wa fedha za Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kwa miradi ya Sekta ya Uchukuzi umeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 6** cha Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

F.3. SEKTA YA MAWASILIANO (FUNGU 68)

51. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi bilioni 18.104** za Sekta ya Mawasiliano zinajumuisha **Shilingi bilioni 4.104** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi bilioni 2.267** ni za Mishahara ya

Watumishi na **Shilingi bilioni 1.837** ni za Matumizi Mengineyo. **Shilingi 14** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, zikiwa ni fedha za ndani.

52. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Mawasiliano, imepanga kutekeleza Mpango wa Muda wa Kati na Muda Mrefu ambao umetilia mkazo katika maeneo yafuatayo:

TEHAMA

i. Utekelezaji, uendeshaji na uendelezaji wa mradi wa ujenzi wa mkongo wa Taifa wa mawasiliano na kufikisha huduma zake hadi makao makuu ya Wilaya zote nchini na ujenzi wa vituo viwili (2) vya kutunzia data (Data Centre) - Dodoma na Zanzibar;
ii. Ujenzi wa Muundombinu wa mawasiliano ya mitandao “Public Key Infrastructure - (PKI)”;
iii. Kuratibu matumizi ya huduma za TEHAMA nchini (National IT systems and services/applications);
iv. Kusimamia utekelezaji wa mkakati wa kitaifa wa usalama wa mitandao (National Cyber security strategy); na
v. Kusimamia uanzishwaji wa mkakati wa mtandao wa TEHAMA wenye kasi zaidi (National Broadband Strategy).

MAWASILIANO

i. Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016; Kukamilisha uhuishaji wa Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003 na Mpango Mkakati wake wa utekelezaji;
ii. Kukamilisha mpango mkakati wa utengenezaji wa vifaa vya TEHAMA nchini na kusimamia utekelezaji wake; na

iii. Kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Anwani za Makazi na Postikodi katika miji mikuu ya mikoa mbalimbali.

53. ***Mheshimiwa Spika,*** mpango wa utekelezaji kazi katika Taasisi zilizo chini ya Sekta ya Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 umeainishwa katika Kitabu cha Hotuba ya bajeti ya Wizara yangu kuanzia **ukurasa 198** hadi **205**.

D. SHUKURANI

54. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaendelea kuwashukuru sana viongozi wenzangu katika Wizara nikianzia na Mheshimiwa Mhandisi Edwin A. Ngonyani (Mb.), Naibu Waziri; Mhandisi Joseph M. Nyamhanga, Katibu Mkuu (Ujenzi), Mhandisi Dkt. Leonard M. Chamuriho, Katibu Mkuu (Uchukuzi), Mhandisi Dkt. Maria L. Sasabo, Katibu Mkuu (Mawasiliano), Mhandisi Angelina Madete, Naibu Katibu Mkuu (Mawasiliano), Wakuu wa Idara/Vitengo; Wenyeviti wa Bodi zilizo chini ya Wizara; Viongozi wa Taasisi na wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano wanaonipatia pamoja na kujituma kwao katika utekelezaji wa majukumu yao.

55. ***Mheshimiwa Spika,*** nachukua fursa hii kuwashukuru washirika mbalimbali wa maendeleo ambao wametoa michango yao kwa namna moja au nyingine katika kuendeleza sekta za Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano hapa nchini. Washirika hao ni pamoja na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), Japan (JICA), Korea Kusini (KOICA), Abu Dhabi Fund, Ujerumani (KfW), Uingereza (DFID), Uholanzi (ORIO), Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), Benki ya Uwekezaji ya

Ulaya (EIB), Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID), Kuwait (KFAED), Uturuki, OPEC Fund, BADEA, HSBC, TMEA, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Sekretarieti ya Jumuiya ya Nchi za SADC, CRDB, TIB, Asasi Zisizokuwa za Kiserikali pamoja na sekta binafsi.

E. MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA YA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILANO KATIKA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/2018, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 4,516,883,061,000.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,929,705,714,000.00** ni kwa ajili ya Fungu **98** - Ujenzi, **Shilingi 2,569,073,208,000.00** ni kwa ajili ya Fungu **62** - Uchukuzi na **Shilingi 18,104,139,000.00** ni kwa ajili ya Fungu **68**- Mawasiliano. Mchanganuo wa fedha zinazoombwa umeonyeshwa kwa kina katika Kitabu cha Hotuba ya bajeti ya Wizara yangu kuanzia **ukurasa 212** hadi **213**.

56. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na hotuba hii, nimeambatanisha Miradi ya Wizara itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2017/2018 (**Kiambatisho Na. 1 - 7**) ikiwa ni pamoja na kiasi cha fedha kilichotengwa kutekeleza miradi hiyo. Naomba **viambatisho** hivyo vichukuliwe kama sehemu ya vielelezo vya hoja hii.

57. ***Mheshimiwa Spika,*** mwisho, napenda nitoe tena shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge wote

kwa kunisikiliza. Hotuba yangu inapatikana katika tovuti ya Wizara: www.mwtc.go.tz na kupitia blog hii: wizarauumtanzania.blogspot.com

58. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja.